

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA SABA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA KWANZA

4 APRILI, 2017

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KWANZA TAREHE 4 APRILI, 2017

I. WIMBO WA TAIFA:

Saa 3.00 asubuhi Wimbo wa Taifa uliimbwa na Dua kusomwa na Mhe. Job Y. Ndugai (Spika)

Makatibu Mezani:

- 1.
2.

II. KIAPO CHA UAMINIFU:

Mhe. Salma Rashid Kikwete aliapa Kiapo cha Uaminifu.

III. TAARIFA YA SPIKA:

Taarifa ya Miswada iliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wa Sita wa Bunge ambayo imepata kibali cha Rais na sasa ni Sheria za nchi. Miswada na Sheria hizo ni:-

- i. Muswada wa Huduma ya Msaada wa Kisheria wa Mwaka 2016, sasa ni Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya mwaka 2017
- ii. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa 2016, sasa ni Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 ya mwaka 2017

Wageni

Mhe. Spika alimtambulisha Bungeni Mhe. Rais Mstaafu Mhe. Jakaya M. Kikwete na Waheshimiwa Wabunge walishangilia kwa muda mrefu kwa kupiga makofi.

IV. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa:-

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA)

Swali Na. 1: Mhe. Khalifa M. Issa

Nyongeza: Mhe. Khalifa M. Issa
Mhe. George M. Lubeje
Mhe. Mch. Peter S. Msigwa
Mhe. Kabwe Z. Zitto

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Swali Na. 2: Mhe. Amina S. Mollel

Nyongeza: Mhe. Amina S. Mollel
Mhe. Juma S. Nkamia
Mhe. Cecilia D. Paresso

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Swali Na. 3: Mhe. Boniface M. Getere

Nyongeza: Mhe. Boniface M. Getere
Mhe. Munde T. Abdallah

Swali Na. 4: Mhe. Leah J. Komanya

Nyongeza: Mhe. Leah J. Komanya
Mhe. Joseph Msukuma

WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Swali Na. 5: Mhe. Ignas A. Malocha

Nyongeza: Mhe. Ignas A. Malocha

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali Na. 6: Mhe. Kasuku S. Bilago

Nyongeza: Mhe. Kasuku S. Bilago
Mhe. Nape M. Nnauye

Swali Na. 7: Mhe. Joyce B. Sokombi

Nyongeza: Mhe. Joyce B. Sokombi
Mhe. Esther N. Matiko

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Swali Na. 8: Mhe. Bhagwanji M. Meisuria

Nyongeza: Mhe. Bhagwanji M. Meisuria
Mhe. Maryam Msabaha
Mhe. Jaku H. Ayoub

Swali Na. 9: Mhe. Anne K. Malecela

Nyongeza: Mhe. Anne K. Malecela

V. MATANGAZO

Mama Tunu Pinda pamoja na Wageni wengine waliokuwa Bungeni walitambulishwa.

VI. HOJA YA KUTENGUA KANUNI

Kanuni ya 28(2) ilitenguliwa ili Bunge lirejee saa 10.00 jioni badala ya 11.00 jioni kwa siku hiyo na pia Bunge likutane siku ya Jumamosi ili kukamilisha shughuli zilizopangwa.

VII. KUSITISHA BUNGE

Saa 10:50 asubuhi Bunge lilisitishwa mpaka saa 10:00 jioni.

VIII. BUNGE KUREJEA

Saa 10:00 jioni Bunge lirejea.

IX. UCHAGUZI WA WABUNGE WA AFRIKA MASHARIKI

- i. Mhe. Spika alitoa maelezo kuhusu utaratibu wa kupiga kura katika uchaguzi wa nafasi za Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki.
 - ii. Katibu wa Bunge alitoa Taarifa kuhusu uteuzi wa Wagombea wa Ujumbe wa Bunge la Afrika Mashariki.
 - iii. Wabunge wafuatao walismama na kuomba kuhusu utaratibu wa zoezi la uchaguzi.
1. Mhe. Jaku Hashimu Ayoub – alitaka kujua kama zoezi hilo la uchaguzi wa EALA linaonyeshwa live na Televisheni.

Spika alijibu zoezi hilo linaonyeshwa na Watanzania wanaona.

2. Mhe. Hamidu Hassan Bobali – aliulizia kuhusu mgogoro wa Chama cha CUF na uamuzi wa pande mbili za CUF kuleta wagombea.

Spika alijibu kuwa suala hilo liko Mahakamani kwa hiyo Bunge lisiingilie.

3. Mhe. John John Mnyika – alieleza kuhusu kitendo cha Chama cha CUF kuleta Wagombea wanne badala ya watatu wanaotakiwa Kikanuni.

Katibu wa Bunge alijibu kwamba Wagombea wote wameletwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

4. Mhe. Katani A. Katani alitaka kujuu kuhusu barua yake ya kutambua/kutotambua Wagombea aliopewa. Spika alieleza kuwa barua hiyo imefutwa.
5. Mhe. Tundu A. Lissu aliuliza mamlaka ya kupokea Wagombea wengine wa CUF zaidi ya wale wanaotambuliwa na CUF ya Maalim Seif yametoka wapi na kwamba hao walioletwa wameletwa na Katibu yupi.

Spika alimtaka Mbunge asome vizuri barua yake.

6. Mhe. George B. Simbachawene na Mhe. Jenista J. Mhagama walismama kuelezea utaratibu unaopaswa kufuatwa kupigia kura kwa majina ya CHADEMA. Hii ni kufuatia Wabunge wa CHADEMA akiwemo Kiongozi wa Upinzani kutaka Wabunge wao wawili wapite bila kupingwa.

Baada ya miongozo hiyo Wagombea wafuatao waliitwa kujieleza na kuulizwa maswali:-

1. Abdullah Hasnuu Makame
2. Mohammed Yusuf Nuh
3. Fancy Haji Nkuhi
4. Happiness Elias Lukigo
5. Happiness Ngoti Mgalula
6. Zainab Rashid Mfaume Kawawa
7. Habib Mohamed Mnyaa
8. Sonia Jumaa Magogo
9. Thomas D.C. Malima - alijitoa
10. Twaha Issa Taslima
11. Maryam Ussi Yahya

12. Rabia Hamid Mohamed
13. Adam Omar Kimbisa
14. Anamringi Issay Macha
15. Charles Makongoro Nyerere
16. Ngwaru Jumanne Maghembe
17. Ezekia Dibogo Wenje
18. Lawrence Kego Masha

Kabla ya zoezi la kupiga kura na maelezo ya zoezi la kupiga kura kutolewa, Wabunge kadhaa waliomba kuhusu utaratibu wa kupiga kura na Wagombea wa CHADEMA kupidwa bila kupingwa au kuhojiwa na Bunge.

Baada ya mjadala kuhusu utaratibu wa kupiga kura, uamuzi ulifikiwa kuwa zipigwe kura za siri. Kura zilipigwa, kuhesabiwa na matokeo kutangazwa kwa wafuatao:-

1. Fancy Haji Nkuhi
2. Happiness Elias Lukigo
3. Abdullah Hasnuu Makame
4. Maryam Ussi Yahya
5. Habib Mohamed Mnyaa
6. Adam Omar Kimbisa
7. Ngwaru Jumanne Maghembe

Wagombea wawili wa CHADEMA hawakupitishwa na Bunge.

X. **KUAHIRISHA BUNGE**

Saa 7:00 usiku Bunge liliahirishwa hadi tarehe 5 Aprili, 2017 asubuhi.